**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**S. L.P. 1575**
**Simu: 028-2700157**
**Nukushi: (028) 2703014**
**Baruapepe:** rbciringa@pccb.go.tz
**Website**: www.pccb.go.tz

**IRINGA, APRILI, 2022.**

# TAKUKURU INAYOTEMBEA YALETA MATOKEO CHANYA KATIKA KUZUIA RUSHWA KATIKA MINADA.

**Ndugu Wanahabari,**
Kwanza kabisa tumshukuru Mwenyezi Mungu kutukutanisha nanyi leo hii kwa ajili ya kuwapeni taarifa ya kazi zilizotekelezwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi, 2022. Taarifa hii inatokana na ofisi ya Mkoa na zile za wilaya za Mufindi na Kilolo, ambapo kazi mbalimbali zimetekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marejeo ya mwaka 2019 kwa lengo la kuhamasisha na kukuza utawala bora na kuondoa rushwa.

Kazi hizi zimetekelezwa kupitia njia ya Uelimishaji ili kushirikisha wadau mbalimbali katika Mapambano dhidi ya Rushwa; lakini pia kwa njia ya Uzuiaji wa vitendo vya rushwa kwa kuziba mianya inayochangia uwepo wake; Pamoja na kupambana na wahalifu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na makosa yahusianayo kwa kufanya chunguzi zinazopelekea kufungua mashtaka Mahakamani.

**Ndugu Wanahabari,**
**UELIMISHAJI UMMA**:

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 Elimu ya mapambano dhidi ya rushwa imetolewa katika makundi mbalimbali ili ***kuhamasisha umma***

***kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa***. Ubunifu na mbinu mbalimbali za kuelimisha zimetumika ikiwa ni pamoja na kuwafikia Wadau moja kwa moja ili kupata mrejesho wa huduma zinazotolewa na Watumishi wa Umma na kama kuna vitendo vya rushwa vinatendeka. Katika ubunifu huu mnamo tarehe 10/03/2022 Maafisa wa TAKUKURU mkoa wa Iringa waliweza kufika katika eneo la Mnada wa ng'ombe, mbuzi na kondoo katika kijiji cha Mnadani Kata ya Izazi wilaya ya Iringa na kupokea kero mbalimbali ambazo walizifanyia kazi.

Pia TAKUKURU iliwashirikisha Wadau katika Mapambano Dhidi ya Rushwa katika kurusha vipindi vya redio ambavyo lengo ni kuwahabarisha wananchi kuhusu kazi inazofanya. Kwa kushirikiana na Afisa Mifugo, Skauti na Wanaklabu za wapinga rushwa wananchi walipata nafasi ya kupiga simu redioni na kuuliza maswali na pia kutakiwa kutoa taarifa za ubadhirifu au ukiukaji wa Maadili ya Utumishi kwa kupiga simu namba 113 au namba ya Kamanda wa TAKUKURU wa mkoa. Pamoja na mbinu hizo, zimefanyika semina **46**, mikutano ya hadhara **48**, uimarishaji wa Klabu za Wapinga Rushwa **67** katika shule za Msingi na Sekondari, Habari **01**, vipindi vya redio **05**, Mkutano na waandishi wa habari **01**, na kugawa machapisho mbalimbali kwa wananchi yenye ujumbe wa kukemea vitendo vya rushwa.

Aidha katika kuzuia vitendo vya rushwa katika Taasisi za Umma, elimu ya Maadili ya Utumishi wa Umma imetolewa kwa Watumishi wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) wa Ofisi ya mkoa wa Iringa, Kilolo na Mufindi kuhusu umuhimu wa kusimamia miradi ya maji na mapato ya Serikali. Pia Jeshi la Akiba Mkoa wa Iringa nao walipata elimu ya Maadili ya Utumishi wa Umma ili kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu.

**Ndugu Wanahabari,**

**UZUIAJI RUSHWA:**

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 TAKUKURU Mkoa wa Iringa imefanya kazi ya Uzuiaji wa vitendo vya Rushwa kwa kuendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na Miradi ya fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 ambayo ipo katika Mkoa wetu.

Jumla ya miradi ya maendeleo **09** yenye thamani ya Shilingi **3,485,161,400** ilikaguliwa katika Sekta za Elimu, Afya na Ujenzi. Katika ukaguzi huo, hakukuwa na miradi iliyokuwa na kasoro hadi katika hatua iliyofanyiwa ufuatiliaji, kazi ya ufuatiliaji inaendelea hatua kwa hatua.

Vilevile zimefanyika chambuzi **06** zilizohusu Idara za Utumishi, Elimu, Madini na Ujenzi katika Manispaa ya Iringa, Wilaya ya Iringa, Kilolo na Mufindi. Lengo la kufanya chambuzi hizi ni kubaini mapungufu yanayoweza kujitokeza katika ukiukaji wa Maadili ya utumishi wa Umma, taratibu za utendaji kazi na upotevu wa mapato ya Serikali. Matokeo ya tafiti hizi yamesaidia kushauri na kurekebisha mifumo mbalimbali ya Idara za Serikali na kuzuia mianya ya rushwa. Mapendekezo ya chambuzi hizi yanasaidia kuboresha Mifumo husika.

**Ndugu Wanahabari,**

**UCHUNGUZI NA MASHTAKA:**

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 tumeendelea kupokea malalamiko na kisha kufanya Uchunguzi. Malalamiko **35** yalipokelewa ambapo malalamiko **23** yalihusu rushwa na **12** siyo rushwa. Malalamiko **12** yasiyohusu rushwa yametolewa ushauri na kufungwa. Taarifa zilizohusu rushwa zimefunguliwa majalada na uchunguzi wake unaendelea pia jumla ya kesi kesi mpya **02** zilifunguliwa, kesi **02** zilitolewa maamuzi na Jamhuri kushinda zote na kesi **12** zinaendelea Mahakamani.

**Ndugu Wanahabari,**

**KAZI KUTOKANA NA TAKUKURU INAYOTEMBEA**

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 ofisi iliendelea na utaratibu wa kusikiliza kero za wananchi kwa kuwafikia katika maeneo yao na kusikiliza kero zao kwa utaratibu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA kwa kufanya mikutano ya hadhara. Mikutano ilifanyika katika vijiji vya Mbugani Kata ya Mboliboli na Mnadani Kata ya Izazi. Wananchi walionesha mwamko mkubwa na ari ya kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU katika kuainisha kero zao zilizohusu rushwa na kuomba utaratibu huu wa kuwafuata katika maeneo yao uendelee ili kutatua kero zao kwa haraka. Mbali ya kupokea kero zao na kuzipatia ufumbuzi, TAKUKURU pia iliwapa elimu wananchi juu ya dhana ya rushwa, umuhimu wa

kusimamia miradi ya maendeleo, umuhimu na jinsi ya kutoa taarifa za vitendo vya rushwa.

**Ndugu Wanahabari,**

**UTEKELEZAJI WA MPANGO KAZI WA TAKUSKA**

TAKUKURU inashirikiana na SKAUTI (TAKUSKA) katika mapambano dhidi ya rushwa. Ushirikiano huu ni kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 inayoitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kushirikiana na wadau mbalimbali katika kukabiliana na rushwa nchini. Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2022 TAKUKURU Mkoa wa Iringa imetekeleza Mpango Kazi wa TAKUSKA kwa kuzindua mafunzo kwa Walezi na Wakufunzi wa Skauti wa wilaya ya Iringa, Kilolo na Mufindi. Baada ya mafunzo hayo Skauti watashirikiana na TAKUKURU kuelimisha katika ngazi zote ili kuwajenga vijana kimaadili na kuwajengea uzalendo. Kwa upande mwingine Skauti pia wameshirikishwa na TAKUKURU katika Mahafali ya Wanaklabu wa Kidato cha sita.

**Ndugu Wanahabari,**

**MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI, MACHI 8, 2022**

Katika kipindi cha Januari hadi Machi TAKUKURU mkoa wa Iringa imeshiriki maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani yenye na Kauli Mbiu **"Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu"**, Machi 08, 2022 kwa kushiriki maandamano yaliyoanzia Viwanja vya Manispaa ya Iringa hadi Viwanja vya Mwembetogwa katikati ya mji wa Iringa.

Katika maadhimisho hayo TAKUKURU ilitoa msaada kwa Watoto Yatima katika kuwatambua Wadau Wenye mahitaji maalum wanaoshirikiana na TAKUKURU katika Mapambano Dhidi ya Rushwa.

**Ndugu Wanahabari,**

**MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA NCHINI**

TAKUKURU Mkoa wa Iringa katika kipindi hiki cha Januari hadi Machi 2022 imeshiriki katika Maadhimisho ya Wiki ya Sheria iliyoanza tarehe 23 Januari, 2022 hadi 29 Januari, 2022 kwa Kauli Mbiu isemayo ***"Zama za Mapinduzi ya Nne ya Viwanda; Safari ya Maboresho Kuelekea Mahakama Mtandao"*** ambapo TAKUKURU ilishiriki katika maonesho yaliyofanyika Viwanja vya Manispaa ya Iringa.

**Ndugu Wanahabari,**

**MKAKATI WA APRILI HADI JUNI, 2022**

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2022 TAKUKURU mkoa wa Iringa imejipanga kuendelea kutatua kero za wananchi zinazohusiana na vitendo vya Rushwa, kutoa elimu kwa wananchi, kuwashirikisha vijana wa Skauti na Wanaklabu za Wapinga Rushwa Mashuleni na Vyuoni katika mapambano dhidi ya rushwa. Vilevile tumejipanga kuendelea kuwaelimisha watumishi wa Sekta za Umma na Binafsi kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao. Tutaendelea kuwafuata wananchi walipo kupitia utaratibu wa **TAKUKURU Inayotembea** ili kusikiliza na kutatua kero zao zinazohusu rushwa. Pia tutaendelea kufuatilia na kuzuia mianya ya rushwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Ndugu Wanahabari,**

**WITO KWA WAKAZI WA MKOA WA IRINGA.**

TAKUKURU Mkoa wa Iringa inatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa sahihi za vitendo vya rushwa kwa kupiga namba 113, kutuma ujumbe mfupi kwa kutumia namba *113#. Pia tunawasihi mjihadhari na watu wanaojifanya Maafisa wa TAKUKURU na kutoa taarifa pale wanapowabaini.

Vilevile, tunawaasa watumishi wote kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao wanapotoa huduma kwa wananchi.

***"KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU"***

Imetolewa na:

Domina J. Mukama,
**Mkuu wa TAKUKURU (M) Iringa**,
Simu: 0738150054